**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 07 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

160. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Idara Maalumu za SMZ zimekuwa zikifanya kazi kubwa katika kazi za ulinzi na usalama wa nchi yetu, pamoja na kufanya bidii katika shughuli za uzalishaji mali ambazo zikipewa msukumo zinaweza kuongeza pato kubwa nchini.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini gani kwenye maeneo ya uzalishaji ya Idara Maalumu na kuwaongezea mitaji, nyenzo na utaalamu ili uzalishaji wao katika maeneo ya kilimo, viwanda na biashara ulete tija zaidi.

(b) Ni kiasi gani cha mapato kwa mwaka kinapatikana katika shughuli za uzalishaji za Idara Maalumu za SMZ.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

109. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kipindi kirefu sasa mfuko wa barabara umeahidi kujega mitaro ya maji ya mvua katika barabara ya Mambosasa kwa Zube, ili kuondoa kadhia ya mafuriko wakati wa kipindi cha mvua katika eneo hilo.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

189. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika malengo ya uhifadhi na maendeleo ya misitu kwa mwaka 2020/2021 ni kufanya utafiti wa kujua idadi ya wanyama adimu na mazingira yao wakiwemo paa nunga, popo wa Pemba na paa chesi wa Pemba.

(a) Je, malengo hayo unayafahamu.

(b) Je, ni idadi gani ya popo wa Pemba waliopo hadi sasa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

52. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Baadhi ya wananchi wa Shehia za Kama, Chuini na Kihinani katika Jimbo la Mfenesini wanaojishughulisha na kazi ya uvuvi hukumbwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya uvuvi kama boti, nyavu na vifaa vyenginevyo.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhusu utafutaji wa soko kwa wananchi wanaofanya biashara ya uvuvi na uuzaji wa dagaa katika maeneo ya Kihinani.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

35. Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Licha ya jitihada kubwa za Serikali katika sekta ya michezo, taswira inaonesha kuwa mchezo wa mpira wa miguu umepewa kipaumbele zaidi kuliko michezo mingine wakati historia inathibitisha kuwa, nchi yetu ilipata heshima kubwa kupitia michezo hiyo.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuiinua michezo mengine kama riadha, “beach socker” na nage, (hand balls) hasa ikizingatiwa michezo hiyo imeipatia heshima kubwa nchi yetu.

(b) Je, wanamichezo hao, mbali na mpira wa miguu, wategemee nini kupitia bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

167. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Moja ya zao la biashara katika Serikali yetu ni karafuu ambapo sasa tunaelekea katika msimu mkubwa wa mavuno ya zao hilo. Wananchi wa Zanzibar kwa kiwango kikubwa wanategemea sana karafuu katika kujikwamua na maisha yao ya kila siku. Pamoja na kuwa zao hilo ndiyo zao kuu la biashara lakini Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) limeshindwa kufanya manunuzi ya karafuu katika kipindi cha msimu uliopita hali ambayo imepelekea baadhi ya karafuu kuendelea kusalia majumbani

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuelekea katika msimu mkubwa wa uvunaji wa zao la karafuu.

(b) Je, wananchi wategemee nini kutoka Serikalini kuelekea uvunaji wa zao hilo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

203. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna taarifa kuwa katika ujenzi wa barabara ya Kitope Sharifumsa, Serikali ilimpa kazi ya ujenzi wa barabara hiyo mkandarasi aliyeomba kupitia zabuni kwa kiwango kikubwa cha fedha, ukilinganisha na waombaji wengine wa zabuni hiyo, ambao wana uzoefu wa muda mrefu, utaalamu na walioomba kazi hiyo kwa kuahidi kujenga barabara hiyo kwa gharama ndogo.

(a) Je, taarifa hizo ni za kweli.

(b) Ni kigezo gani mahsusi kwa kuzingatia uzoefu na utaalamu kilichotumika kumpata Mkandarasi mjenzi wa barabara hiyo.

(c) Katika kuokoa fedha za Serikali, ni kwa sababu zipi Wizara yako isimpe kazi Mkandarasi mjenzi aliyeomba kwa kiwango cha wastani au kiwango cha chini hasa ukizingatia waombaji wengine wa zabuni hiyo wameshajenga barabara nyingi katika mtandao wa barabara Zanzibar.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

131. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeongeza tahasusi tano (5) mpya katika masomo ya sayansi na masomo ya lugha na wanafunzi wataanza kusoma masomo hayo kuanzia mwaka 2021.

(a) Je, Wizara yako imeshaandaa mazingira ya kufundishia masomo hayo mapya hapa Zanzibar.

(b) Je, kwa mwaka huu wa masomo, somo la lugha ya kichina litafundishwa hapa Zanzibar.

(c) Je, ni skuli gani zilizoandaliwa kufundisha masomo hayo yaliyoongezwa.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

193. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hospitali ya Binguni utafanywa na kampuni ya ujenzi ya Serikali yenye wataalamu wa ujenzi kutoka vikosi vya SMZ.

(a) Je, wataalamu hao watakaotumiwa wana uzoefu wa ujenzi katika kujenga majengo ya hospitali yatakayokwenda sambamba na mahitaji mbali mbali ya hospitali.

(b) Je, kampuni hiyo ina vigezo vya kutosha kupatiwa kazi hiyo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**07 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**